**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

## UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA ILIYOSAMBAA MITANDAONI IKIDAI KUSITISHWA KWA AJIRA MPYA YA VIJANA 19

Hivi karibuni kumekuwepo na taarifa iliyosambaa katika mitandao wa kijamii kuhusu kusitishwa kwa ajira ya vijana 19 ambao walifaulu usaili wa kazi na kuitwa kwenye mafunzo. Taarifa hiyo inaweza kuleta taharuki kwa umma hivyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) inapenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:

Kati ya mwezi Desemba 2025 hadi Februari 2026, TAWA ilipokea watumishi tarajali 295 kutoka Sekretarieti ya Ajira kwa ajili ya mafunzo ya awali ya kijeshi kabla ya kuajiriwa rasmi. Watumishi tarajari wanaporipoti kwa ajili ya mafunzo ya awali ya kijeshi hupaswa kupimwa afya na kufanyiwa uhakiki wa taarifa ikiwemo uhalali wa vyeti vya kuzaliwa na taaluma. Uhakiki uliofanyika umebaini kuwa taarifa za watumishi tarajali 25 kati ya 295 zina dosari mbalimbali, hivyo watumishi hao wamerejeshwa Sekretarieti ya Ajira kwa ajili ya kurekebisha dosari husika. Zoezi hili la uhakiki limezingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na Amri za jumla za Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu.

TAWA inapenda kuufahamisha umma kuwa hadi sasa **HAKUNA** mtumishi tarajali aliyesitishiwa ajira yake kutokana na zoezi la uhakiki linaloendelea katika Kituo cha Mafunzo Fort Ikoma - Serengeti. TAWA inatoa rai kwa umma kuacha kusambaza taarifa zisizo na ukweli ambazo zinalengo la kuichafua taswira ya Mamlaka na Serikali kwa ujumla.

Imetolewa na;

**Kitengo cha Mahusiano kwa Umma – TAWA**
**02.03.2026**